(132)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Mahakama,
S. L. P. 1419,
53103 MBEYA.
Simu: (025) 252503566
Nukushi: (025) 252502958
Barua pepe:
rbcmbeya@pccb.go.tz
Wavuti : http://www.pccb.go.tz

MBEYA AGOSTI –2022

TAKUKURU MBEYA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 10

Ndugu wanahabari,
Leo tumekutana tena katika ofisi yetu ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya ili kupitia ninyi tuweze kuueleza umma kuhusu utendaji kazi wa ofisi yetu kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi wa Aprili hadi Juni 2022.

Kwa mujibu kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329 toleo la mwaka 2019, TAKUKURU inayo majukumu makuu matatu ambayo ni; Kuelimisha Jamii juu ya rushwa na madhara yake; Kufanya chambuzi za mifumo kwenye taasisi za umma na sekta binafsi kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna bora ya kuziba mianya hiyo, pamoja na kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mahakamani kwa maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

UZUIAJI RUSHWA

Kwa upande wa Uzuiaji Rushwa, katika kipindi hiki cha miezi mitatu TAKUKURU Mkoa wa Mbeya imefanikiwa kufanya **chambuzi za mifumo nne (04).** Chambuzi hizi zimefanyika katika Kata za Halmashauri ya jiji la Mbeya na Mbarali. Katika chambuzi hizo,

tulibaini mapungufu hasa kwenye utunzaji sahihi wa taarifa na namna wananchi wanavyoshughulikiwa malalamiko yao. Baada ya uchambuzi huo, TAKUKURU ilikaa vikao na wadau wanaohusika kwenye sekta hizo kwa ajili ya kuweka maazimio ya kuondoa mianya ya rushwa iliyobainika na kuwekeana mikakati ya ufuatiliaji.

Pia, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo **kumi na moja (11)** yenye jumla ya thamani ya shilingi **Bilioni Kumi, Milioni mia tatu kumi na tano, mia tano na tisa mia tisa themanini na tisa na senti thelethini na nne (10,315,509,989.34)**. Miradi hiyo ni ya sekta za Elimu, Maji, na Barabara, hivyo ufuatiliaji ulifanyika wa miradi hiyo kwa lengo kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa ubora uliokusudiwa na kwa thamani halisi ya fedha iliyotolewa na kutumika na pia utekelezaji wake unakamilika ndani ya muda uliopangwa.

Baadhi ya miradi iliyofuatiliwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Mlima reli.

Hata hivyo, baadhi ya mapungufu yaliyobainika katika ufuatiliaji wa miradi hiyo kama vile wakandarasi kuchelewa kuanza kazi mara baaada ya kukabidhiwa mradi, moja ya mambo ambayo yanaweza kusababisha mwanya ya rushwa, yameweza kufanyiwa kazi kwa kufanya vikao na wadau wa miradi husika pamoja na kutoa elimu kwa lengo la kuondoa mianya hiyo na kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kusisitiza uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma ili kupata miradi bora yenye kukidhi thamani ya fedha (Value for money).

ELIMU KWA UMMA

TAKUKURU Mkoa wa Mbeya katika kipindi cha miezi mitatu imeendelea na jukumu la kuelimisha umma kwa kuyafikia makundi mbalimbali ya jamii kwa lengo la kuendelea kuwajengea uelewa wa madhara ya rushwa, ili waweze kushiriki katika mapambano ya vita dhidi ya rushwa.

Kupitia uelimishaji umma, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya imewafikia wananchi wapatao 1,506 ambao walipata elimu ya Kuzuia na

Kupambana na Rushwa, ambapo, semina 12 na mikutano ya hadhara 12 ilifanyika, vipindi vitano vya radio viliandaliwa na pia, ulifanyika uelimishaji kupitia uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa 23 za shule za msingi na sekondari.

TAKUKURU INAYOTEMBEA

Ili kuwafikia wananchi katika maeneo yao, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya inaendelea kuelimisha wananchi kwa kupitia mpango wa TAKUKURU INAYOTEMBEA ambapo wananchi walielimishwa na wao pia kutoa kero walizonazo. Baadhi ya wananchi waliofikiwa ni wa vijiji vya Talatala, Lupaso na Mwaya vilivyoko Mkoa wa Mbeya.

UCHUNGUZI

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya imepokea jumla ya **taarifa mpya 71** za tuhuma za makosa ya rushwa na makosa mengine.

Katika taarifa hizo **71** zilizopokewa, taarifa **49** zilihusu rushwa na taarifa **22** hazikuhusu rushwa. Katika taarifa **49** zilizohusu rushwa, taarifa **42** uchunguzi wake unaendelea na taarifa **07**-Uchunguzi umekamilika. Vilevile, katika taarifa **22** ambazo hazikuhuzu rushwa, watoa taarifa ambao ni wananchi wa Mkoa wa Mbeya walielimishwa na kushauriwa.

MASHTAKA

Kwa upande wa Mashtaka, katika kipindi hicho, kesi **thelathini na moja (31)** ziliendeshwa mahakamani ikiwemo kesi mpya **kumi na tano (15)** zilizofunguliwa katika kipindi hicho. Ambapo kesi **kumi (10)** ziliamuliwa na katika kesi hizo kumi zilizoamuliwa, serikali ilishinda kesi **saba (07)** na kushindwa kesi **tatu (03).**

MIKAKATI YETU KWA KIPINDI CHA MIEZI MITATU IJAYO.

Katika kipindi cha miezi mitatu ijayo kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2022 tumejipanga kufanya mambo yafuatayo: -

1. Kuendelea kuelimisha wananchi kuhusu rushwa na madhara yake katika usimamizi wa miradi ya maendeleo katika kata, vijiji na mitaa na kuuboresha mpango wa utoaji Elimu wa TAKUSKA. Lengo ni kuwawezesha wananchi kupata uelewa na kuweza

kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa karibu na weledi wa hali ya juu, Pia, kutoa taarifa TAKUKURU za kutendeka kwa vitendo vya rushwa mara wanapo vibaini.

2. Tutaendelea kufanya kazi za uzuiaji rushwa kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika maeneo mbalimbali hasa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa nia ya kuhakikisha kwamba, fedha za miradi ya maendeleo zinatumika kwa jinsi ilivyokusudiwa, tutaendelea kufanya ufuatiliaji kuhakikisha kwamba thamani ya mradi inaendana na fedha iliyotumika, vilevile kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria watakaobainika kufuja fedha za miradi ya maendeleo.

3. Tutaendelea kufanya uchunguzi na kuwachukulia hatua wale wote watakao kutwa na tuhuma za vitendo vya rushwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani.

HITIMISHO

Tunawapongeza wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa jinsi wanavyoendelea kushirikiana na TAKUKURU katika kufichua vitendo vya rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo hivyo. Tunawasihi waendelee kushirikiana na TAKUKURU kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa nasi tunaahidi kuzifanyia kazi kwa wakati taarifa tutakazo zipokea. Vilevile tunatoa **wito** kwa watendaji wa taasisi zote kusimamia kwa ukamilifu miradi ya maendeleo wanayoisimamia katika maeneo yao.

Aidha, tunatoa ONYO kwa baadhi ya maafisa ardhi wasio waaminifu wanaoshirikiana na wananchi na baadhi watendaji wa mitaa na Kata kuandaa nyaraka za kughushi na kupima maeneo ya umma kwa kusingizia kwamba ni maeneo yao ya asili huku wakijua kwamba si kweli. Tunawaonya waache tabia hiyo mara moja na hatua kali kwa mujibu wa sheria zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika.

Ombi kwa wananchi wote ni kuendelea kutoa taarifa za wale wote wanaojihusha na vitendo vya rushwa kwa njia ya simu ya bure 113, au kufika katika Ofisi za TAKUKURU Mkoa na Wilaya kwa ajili ya kutoa taarifa.

Imetolewa na:

MAGHELA NDIMBO
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA
Nambari ya simu: SIMU BURE 113
MKUU WA TAKUKURU (M) 0738 150 137
NAIBU MKUU WA TAKUKURU (M) 0738 150 138